# KUHUSIANA NA WATU *KWA*

# MIPAKA



JAMES KALEKWA

# KUHUSIANA NA WATU KWA MIPAKA.

James Kalekwa

# Orodha ya Yaliyomo

Maisha ya mwamini na watu wote .......................................... 4

Mizigo na Furushi .............................................................. 5

Kilelezo cha Mahusiano cha Yesu [The Jesus Friendship/Relation Model] ................................................... 7

I. Makutano ...................................................................... 8

II. SABINI ......................................................................... 11

III. WAFUASI ................................................................ 12

IV. THENASHARA ........................................................ 15

V. MDUARA WA NDANI ................................................ 17

VI. MWANAFUNZI ALIYEMPENDA ............................. 19

HITIMISHO ........................................................................ 20

Kuhusu Mwandishi: ............................................................ 21

Kuhusu New Vine Church: .................................................. 22

Mawasiliano na Mwandishi: ................................................ 22

## Maisha ya mwamini na watu wote

Mtu yeyote aliyeokoka anahitajika kuwa na mahusiano mazuri na watu wote.

"Tena haimpasi mtumwa wa Bwana kuwa mgomvi; bali kuwa mwanana kwa watu wote, awezaye kufundisha, mvumilivu;" **2 Timotheo 2:24**

"Kama yamkini,kwa upande wenu, make katika Amani na watu wote." **Warumi 12:18**

"Tafuteni kwa bidii kuwa na Amani na watu wote, na huo utakatifu, ambao hapana mtu atakayemwona Bwana asipokuwa nao;" **Waebrania 12:14**

Kwa msingi wa neno, Mungu anatutarajia waamini kama mtu mmoja mmoja kuwa katika hali ya amani/mwanana kimahusiano na watu wengine.

Ikitokea kuna watu wanakuchukia, hawapatani na wewe, ni maaduni. Neno la Kristo linaelekeza namna ya kuishi na adui.

"Lakini mimi nawaambia, wapendeni adui zenu, waombeeni wanaowaudhi" **Mathayo 5:44**

Mungu anatutarajia kuwapenda maadui na kuwaombea wale wanaotuudhi. Si chini au pungufu ya hapo.

Mungu anatutarajia kuwaheshimu watu wote na kuwapenda ndugu [waamini].

“Waheshimuni watu wote. Wapendeni ndugu. Mcheni Mungu. Mpeni heshima mfalme.” **1 Petro 2:17**

Hata hivyo, pamoja na yote hayo, Mungu hatutarajii vile vile kuhusiana na watu wote kwa namna ileile na kwa ngazi ileile. Ukifuatilia kwenye neno la Kristo, utagundua ya kwamba kuna ngazi za kuhusiana na watu na namna za kuhusiana na watu kwenye kila ngazi.

Kiwango hicho cha mahusiano, ngazi na namna ya kuhisana na watu huamia pia matarajio yako kwao [yaani, wajibu wao kukuelekea wewe]; na matarajio yao kwako [yaani, wajibu wao kuwalekea wao].

## Mizigo na Furushi

Nimewahi kushangazwa sana na andiko hili. Na kutokea hapo nikagundua mambo kadhaa kuhusu mahusiano yangu binafsi na watu wengine.

“2. Mchukuliane mizigo na kuitimiza hivyo sheria ya Kristo.

“5. Maana kila mtu atalichukua furushi lake mwenyewe.” Wagalatia 6:2,5

Kuna mambo kwenye maisha ambayo yanakidhi kigezo cha kuwa mzigo. Kwa mujibu wa neno la Mungu, haya yanapaswa kuchukuliwa kwa kusaidiana. Hata hivyo, kuna mambo ambayo ni furushi ambayo yanapaswa kuchukuliwa na mtu binafsi/muhusika.

Ukiitambua siri hii itakupunguzia maumivu ya nafsi na kukatishwa tamaa na watu wengine. Kimsingi, kuumizwa moyo ni matokeo ya kuwa na matarajio ya hali ya juu sana kuwalekea watu wengine ambao hukupaswa kuhusiana nao kwa ngazi na namna hiyo. Upande wa pili, siri hii itakuepusha kuingia kwenye orodha ya watu uliowaumiza kwa kutowatimizia kile walichokitarajia kutoka kwao [wajibu wako kuwalekea wao].

Mwaka 2015, mimi na mke wangu tulipita kwenye moja ya nyakati zilizotusaidia kuwa watu bora na thamani sana. Tulipita kwenye *“defining moment”* – kwenye bonde la uvuli wa mauti. Ilitusababisha tutulie na kuohoji mambo mengi sana. Kupitia maombi na kutafuta kufahamu zaidi, ndipo Roho Mtakatifu alitufunulia jambo ambalo nitatumia muda mrefu kwenye kitabu hiki kulifundisha. Ni namna gani Yesu Kristo akiwa hapa duniani aliishi kama mwanadamu na kuhusiana na watu wote.

## Kilelezo cha Mahusiano cha Yesu [The Jesus Friendship/Relation Model]

- Yesu aliwagawa/aliwapangilia watu na namna ya kuhusiana nao baada ya kujitambua YEYE ni nani na si kwa kutazama wao ni akina nani.

- YEYE ndiye alikuwa mwamuzi wa mahusiano – ni kwa ngazi gani ahusiane na akina nani na ahusiane nao kwa namna gani [Yaani, awe na matarajio gani na abebe wajibu gani kuwaelekea].

- Aliwapangilia kwenye madaraja [levels] mbalimbali ambayo pia yanaonyesha namna gani alihusiana nao; Tuliamua kuiita namna hii ya Yesu kuhusiana na watu *"The Jesus Friendship/Relation Model"*


- Maandiko Matakatifu yanasema hivi:

"…akawaita wale ALIOWATAKA MWENYEWE." (Marko 3:13)

- Kwenye swala la kuhusiana na watu, Yesu hakuwa "passive"; hakutulia tu na kuyaacha mambo yamtokee kama muhanga. Aliamua maisha yake yaweje kwenye eneo hili.

Baada ya kufunuliwa jambo hili, na kulisoma kwa undani na kukaa nalo kwenye maombi na utekelezaji.

Tulichagua kuliweka kwenye kielelezo rahisi na Ufupisho wa fundisho lote kwa mchoro mmoja.




**Mchoro: Kielelezo cha mahusiano cha Yesu**

Sehemu zinazofuata za kitabu hiki ninawekeza kufafanua kila kipengele na kutoa ushauri.

## I. Makutano

*"Naye Yesu akajitenga, yeye na wanafunzi wake, akaenda baharini. Mkutano mkuu wakamfuata, kutoka Galilaya na Uyahudi."* **Marko 3:7**

Hili ni andiko moja kuwakilisha maandiko mengi kwenye vitabu vya injili. Ukisoma kwa mfano, injili kama ilivyoandikwa na Mathayo pekee, watu wanaotajwa kama makutano [kwa kuhusianishwa na Yesu] wanatokeza mara 32 [Biblia Takatifu SUV]

Ni kundi ambalo kila msomaji wa Biblia analifahamu au amewahi kulisikia.

Ukilifunua kundi hili utagundua kuna muunganiko wa watu kutoka sehemu mbalimbali za kijiografia, kihistoria, kimaisha na kiimani. Lilikuwa ni kama kapu la kukusanya watu wote.

Hawa ni watu waliomfuata Yesu wakiwa wamejawa na matarajio mengi kumuhusu. Wengine walienda kumuona na kumshangaa ni mtu wa namna gani; wengine walimwendea wakiwa na mahitaji ya kiafya – magonjwa, ulemavu; wengine walimfuata wakiwa na dhiki nyingi za kimaisha. Na kuna wengine walienda ili kumchunguza, kumdadisi na huenda wapate jambo lakumshtaki nalo kwenye mabaraza ya dini na mamlaka za kiserikali. Pia, kulikuwa na watu waliotaka kumshusha/kumdhalilisha mbele ya umati kwa kuonyesha kwamba mafundisho yake si kitu… kuna watu ambao kwakweli walikuwa hawana pa kwenda, walikuwa wanaenda kupumzikia/kupotezea muda kwa Bwana Yesu.

Kimahusiano, hata wewe una watu ambao watakuja kuhusiana na wewe kutokea kwenye makundi kama niliyoyaanisha hapo juu.

Kama ambavyo Bwana Yesu hakuwatupa kule, kuwadharau au kuwaona hawafai. Bali alihusiana nao na kutumia muda pamoja nao. Ndivyo nawe unapaswa kufanya.

Sasa, tazama ni kwa namna gani Yesu alihusiana nao.

- **WAJIBU WAO:**
  - ✓ Hawana wajibu wowote kukuelekea wewe. Kwa hiyo, usiwe na matarajio yoyote kwao.
- **MATARAJIO YAO:**
  - ✓ Kupokea miujiza
  - ✓ Kulishwa mikate
  - ✓ Watu wao kuhudumiwa/kutendewa
  - ✓ Kusikilizwa, kujaliwa na kujibiwa maswali
- **USHAURI:**
  - ✓ Acha waone matokeo na matukio – inawatosha

✓ Usiache kuwatendea yaliyo ndani ya mkono wako [kutana na mahitaji yao kwa kadiri ya neema uliyopewa]

## II. SABINI

"Basi baada ya hayo Bwana aliwaweka na wengine, sabini, akawatuma wawili wawili wamtangulie kwenda kila mji na kila mahali alipokusudia kwenda mwenyewe." **Luka 10:1**

Kuna kundi la watu ambalo linajitokeza kwenye Maandiko Matakatifu na hutambulishwa kwa jina la "Sabini". Hili ni kundi ambalo lilikuwa limesogelea Yesu kiasi cha kuaminiwa na kupewa baadhi ya majukumu/kazi. Kimsingi, ni duara la kazi.

Kama ilivyokuwa kwa Yesu, nawe unaweza kuwapanga watu kwenye kundi hili. Si lazima wawe sabini kiidadi bali mkazo uko kwenye ngazi na namna ya kuhusiana nao. Huoni mahusiano ya Yesu na kundi hili nje ya "kazi maalum"

Hawa ni wafanyakazi wenzako (colleagues), ni watu uliosoma nao ngazi yoyote ile ya elimu (mates), ni watu mnaofanya nao mradi.

- **WAJIBU WAO:**

- ✓ Kutenda na kutimiliza kazi inayowaunganisha (mradi, ajira, masomo n.k) – msiende zaidi ya hapo, mtaharibu kazi, mtaharibu mahusiano yenu na maswala mengine. Husianeni kikazi.
- ✓ Kutunza mahusiano ya kazi [Baada ya kumaliza kazi warurdi kutoa taarifa ya "mradi wa Injili"]

- **MATARAJIO YAO:**
  - ✓ Ushirikiano kutimiliza jukumu. Unapaswa kuwepo, kupatikana na kushiriki kwenye kazi inayowaunganisha.

- **USHAURI:**
  - ✓ Usichanganye mambo ya kazi na mambo binafsi, ndoa, familia – Huwa ninapenda kukaza hapa kwa kusema *"Ukileta ndoa kazini, itafinyiwa kazi; na baada ya muda utagundua imeisha!"*

## III. WAFUASI

"Akapanda mlimani, akawaita aliowataka mwenyewe; wakamwendea." Marko 3:13

Hili ni kundi ambalo unaweza usilione kwa haraka. Ni kundi lilimsogelea Yesu kwenye maisha yake na kumabatana naye muda mrefu. Ni kundi ambalo linakusanya wale Thenashara na watu ambao huwa ninawaita "kundi kimya" – Martha, Mariam, Lazaro, Mariam wa pili, mama mkwe wa Petro, na wanawake aliowaponya ambao Biblia haiwataji majina.

Kwenye yale maduara mawili ya kwanza, huoni watu wakifanya wajibu wa kuyahudumia au kujitoa kwa ajili ya maisha ya Yesu. Lakini kundi hili lina jambo tofauti.

- **WAJIBU WAO:**
    - ✓ Hutoa muda, mali, vitu – rasilimali zao kufanikisha *"maono yako"* [Maono/Huduma/Kanisa ni la Mungu si mali ya mtu binafsi. Huwa tunashirikishwa tu kuwa sehemu kama watendakazi pamoja na Kristo; ndiyo maana nimeweka *"maono yako"*] – Hili ndiyo kundi ambalo linaandaa chakula, linaingia gharama na kujua kuhusu maisha ya Bwana Yesu.
    - ✓ Kuna watu ambao wapo kwenye maisha yako na wengine ambao watakuja na watajitoa kuyahudumia maisha yako na

mahitaji yako. Walau utapata watu wanaokuwazia na wewe.

- ✓ Hukuamini na kuambatana na wewe.

- **MATARAJIO YAO:**

  - ✓ Waamini Baada ya kuwathibitisha, waamini. Waonyeshe mpaka wajue kwamba unawaamini.

  - ✓ Kasimisha kwao (Delegate) baadhi ya majukumu. Unapopata watu wa namna hii, baadhi wa majukumu unapaswa kuwapatia. Ndivyo alivyofanya Bwana Yesu.

  - ✓ Patikana kwa ajili yao [be available]. Unapaswa kutenga muda kwa ajili yao. Unakumbuka kilio cha Martha miguuni pa Yesu, *"...kama ungalikuwapo hapa, ndugu yangu hangalikufa."* Yohana 12:21b. Huwezi kuwa na ujasiri wa kumlaumu Yesu kiasi hicho kama hamna kiwango cha mahusiano ambayo mnamtarajia atende hivyo. Hii habari tunafahamu ilivyoanza, Lazaro alivyougua tu walimtumia Yesu ujumbe [Yohana 11:3]. Hii ni kuonyesha walikuwa na matarajio na Yesu kwa sababu ya mahusiano yao.

- **USHAURI:**
    - ✓ Watunze na watambue (acknowledge them) sirini na hadharani

## IV. THENASHARA

“13.Akapanda mlimani, akawaita aliowataka mwenyewe; wakamwendea.

14. Akaweka watu kumi na wawili, wapate kuwa pamoja naye, na kwamba awatume kuhubiri

16. Akawaweka wale Thenashara; na Simon akampa jina la Petro.”

Marko 3:13,14,16

Hili ni kundi ambalo analichagua baada tu ya kutoka kwenye mlima wa maombi wa usiku kucha; maombi ya masaa kumi mbili. Unaweza kusema ya kwamba alitumia wastani wa saa moja kuuomba kumpata kila mmoja.

Kwa sababu ya unyeti wa hawa watu; wanaambatana na maisha yake yote na baade anakuja kuiacha kazi mikononi mwao, asingekurupuka tu kuwapata.

Ni watu ambao waliambatana naye kiasi kwamba wakafanana naye [kutembea, kuongea, mavazi]. Si watu wakuokota tu njiani.

Ikumbukwe ya kwamba Yesu tayari alikuwa anafuatwa na watu wengi mpaka hivi sasa. Kupata watu kumi na mbili miongoni mwa watu kumi na tatu si ngumu sana. Kupata kumi na mbili miongoni mwa ishirini na nne na kuendelea ni kazi sana. Si ajabu yalihitajika maombi.

Ili upate watu watakaoyashiriki maisha yako umbali huu, yanahitajika maombi.

- **WAJIBU WAO:**

✓ Kujidhabihu; Kiuhalisia watu hawa wameacha vyote... wameacha kila kitu! Fikiria akina Simoni Petro na Andrea; Yakobo wa Zebedayo na Yohana [Maro 1:16-20]. Waliacha nyavu na shughuli za uvuvi. Lawi mtoza ushuru akiwa katikati ya kazi aliacha na kumfuata Yesu [Luka 5:27]… Si ajabu Petro alimuuliza *"…sisi tumeacha vyote tukakufuata, tutapata nini basi."* Mathayo 19:27. Hiyo sentensi haikuwa ya kufikirika au ya ulimwengu wa roho. Ni kweli walicha vyote!

✓ Kuna kitu tunavuviwa kutokea kwenye swali la Petro. Ni kufanya tathmini ya kimahusiano. Usiayaache mahusiano yaende bila kufanyiwa tathmini/mapitio. Na Yesu hakukasirika wala

kukerwa na swali. Watu waliojidhabihu kiasi hiki wanastahili kuuliza maswali magumu na kujibiwa.

- **MATARAJIO YAO:**

✓ Washirikishe kwenye Mchakato. Hili ni kundi ambalo Yesu alihakikisha wanafahamu yote. Alikuwa radhi kuahirisha mazungumzo na makutano ili awafafanulie hawa jambo.

✓ Wajulishe "technical HOWs" – namna ya kufanya mambo fulani. Hawa ndiyo aliwafundisha kwa maneno na kwa mifano juu ya mambo mbalimbali ya maisha. Kuna mahali anawafundisha namna ya kutoa pepo (moja ya mambo mengi aliyowafundisha). Si watu wengi walipata hii nafasi ya kujua *"namna ya…"* kutoka kwa Bwana Yesu.

- **USHAURI:**

✓ Wasogeze karibu na uwape nafasi stahiki

✓ Wahamasishe (motivate) hamasa ya kweli.

## V. MDUARA WA NDANI

"Wala hakumruhusu mtu afuatane naye, ila Petro, na Yakobo, na Yohana nduguye Yakobo." **Marko 5:37**

Hili ni kundi la watu watatu waliotokea miongoni mwa wale Thenashara. Hawa waliona mambo zaidi ya walioyaona thenashara.

- **WAJIBU WAO:**

✓ Kuona na kutunza mambo ya ndani (Hawa tu ndiyo waliokuwepo kwenye mlima wakati Yesu anaomba mpaka sura na mavazi yake yanageuka; na ndiyo waliokuwepo kwenye maombi machungu ya Gethsemane).

✓ Kuona madhaifu na ubinadamu/ukawaida – walipewa nafasi ya kuona upande wa Yesu akilalamika anahitaji watu waombe pamoja naye; analalamika kwanini wamesinzia; na analalamika na kuomba kikombe kimuepuke; wanamuona anaanguka kifudifudi na anatoa machozi.

✓ Kutunza heshima. Pamoja mambo yote waliyoyaona. Waliendelea kutunza heshima ya Bwana Yesu kati yao na mbele za wanafunzi wengine.

- **MATARAJIO YAO:**

✓ Jiachie/Kuwa wazi kwao (Be vulnerable). Yesu hakujificha kwao; hakuwa fumbo kwao. Alikuwa muwazi. Jambo hili huwa ni “hatari” kidogo. Lakini linapaswa kuwa hivyo.

✓ Waonyeshe mambo ya ndani – magumu, mazito, kukosa majibu, kuumia, hofu n.k

- **USHAURI:**

✓ Watunze na Watambue. Hawa ni watu adimu sana. Ukiwapata, wakumbatie kwa nguvu.

✓ Usiwaingize kwenye vita dhidi ya wengine (Yesu hakuwafunua sana/kuwatambulisha hadharani kwa kila mtu. Jambo hili lingevuta vita kubwa kuwaelekea).

## VI. MWANAFUNZI ALIYEMPENDA

"23. Na palikuwa na mmoja wa wanafunzi wake, ameegama kifuani pa Yesu, ambaye alimpenda. 24. Basi Simoni Petro akampungia mkono, akamwambia, Uliza, ni nani amtajaye?" **Yohana 13:23-24**

Kuegamia kifua cha Yesu! Ni mazoea yaliyopitiliza. Lakini ukweli ndiyo huo. Kuna mtu alikuwa karibu na Yesu kiasi hicho, na huyo mtu si Petro. Kwa kuwa ilikuwa ni siri baina ya Yesu na huyo mwanafunzi, yeyote atakayeisema basi ndiye muhusika. Mwanafunzi huyo ni Yohana. Kimsingi, maelezo juu ya mwanafunzi aliyempenda huyapati mahali pengine popote isipokuwa kwenye injili hii.

- **WAJIBU WAKE:**

✓ Kuona na kutunza mambo ya ndani ya kina zaidi. Fikiria umeagamia kifua. Ni nafasi ya kusikia zaidi

ya yanayosemwa. Ni kusikia mapigo ya moyo, lakini unachagua kuyatunza.

- ✓ Kuona zaidi ya matendo; kusikia zaidi ya maneno – ni muunganiko mkubwa wa kiroho na kihisia. (ili mtu afikie hapo lazima awepo na apatikane – present and available)

  - **MATARAJIO YAKE:**

- ✓ Mpatie nafasi yake stahiki. Mpe “kuegamia kifua”; ndipo mahali anapotakiwa kuwa.
- ✓ Mlinde dhidi ya mashambulizi na ulaghai wa watu wengine.

## HITIMISHO

Baba yangu wa kiroho na Mchungaji wangu Pastor Goodluck Kyara hutufundisha hivi, mahusiano ni mchakato – si jambo la mara moja. Wape watu na mambo muda kujipambanua na kujithibitisha. Usiyaharakishe mambo. Wacha mambo yatiririke au yajiumbe yenyewe.

Nimeazima hekima za baba yangu kutaka kukuonyesha ya kwamba usiwape watu kuingia

kwenye mduara ambao hawakustahili kuwa. Au usiwapandishe vyeo. Mahusiano yenyewe yataendelea mpaka yatafikia mtu kuingia kwenye mduara fulani.

Naomba nikuhakikishie, ukifanya hivyo itakupunguzia maumivu ya nafsi kwa sehemu kubwa sana.

Pamoja na hayo yote tambua kuna nyakati (msimu) za kuachwa, kusalitiwa na kukataliwa – NI KAWAIDA!

Hata hivyo ni vizuri ukajua, wakati unawapanga watu kwenye maduara ya kimahusiano; nao watakuwa wanakupima na kukupanga kwenye duara unalostahili. Wape nafasi na uhuru wa kufanya hivyo.

## Kuhusu Mwandishi:

Mwandishi wa kitabu hiki, James Kalekwa, ni mfuasi wa Yesu Kristo; mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; Mume mpenzi wa Frida, baba anayewajibika wa Joshua-Vision, Charis “Tai”, Victor na Priscilla; na anafurahia kuwa mchungaji mkazi wa kanisa la New Vine jijini Dodoma.

Mchungaji James ameitwa *"Kuujaza ulimwengu kwa maarifa ya utukufu wa Mungu kama maji yaifunikavyo bahari."* [Habakuki 2:14]

## Kuhusu New Vine Church:

Kanisa la New Vine limebeba utume wa kuinua kizazi cha kiungu kitakacholeta mguso chanya kwenye kila nyanja ya maisha kwenye jamii, taifa na mataifa. (Mathayo 5:13-14/Yoeli 2:2-11)

Makao makuu ya kanisa (Gloryland) yako Mwanza chini ya mwangalizi ambaye pia ni muasisi, Mchungaji Goodluck & Mama Ziada Kyara.

Kufahamu zaidi kuhusu kanisa hili kwa ujumla tembelea: https://www.newvinechurch.or.tz

## Mawasiliano na Mwandishi:

Iwapo unahitaji kupata mafundisho zaidi ya maandishi n audios kutoka kwa mwandishi wa Kitabu hiki, Mchungaji James Kalekwa. Unaweza kufanya hivyo kupitia channel ya telegram: https://t.me/nvcdodoma AU fungua app ya telegram kisha tafuta @nvcdodoma

Unaweza pia kumfuatilia mwandishi kupitia mitandao ya kijamii:

Facebook: James Kalekwa

Instagram: james_kalekwa

Twitter: @MchungajiJK

Iwapo una ushuhuda, unahitaji ushauri na msaada wa kichungaji unaweza kuwasiliana naye moja kwa moja kupitia +255-754-917-7764 (Kupiga simu, SMS na WhatsApp)

# KUHUSU MWANDISHI



**James Kalekwa** ni amemwamini Yesu kuwa Bwana na Mwokozi wa Maisha yake. Ni mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; ni mume mpenzi wa Frida; baba anayewajibika kwa Joshua-Vision, Charis "Tai", Victor na Priscilla. Ni mchungaji wa New Vine Church - Dodoma.


James Kalekwa

james_kalekwa

@MchungajiJK

+255 754 917 764